# UAVYAJI MIMBA KWA KUTUMIA DAWA YA MISOPROSTAL

## UFANYAJI KAZI WA DAWA

Misoprostol inafanya kazi ya kukatisha ujauzito kwa takriban wanawake tisa (9) kati ya kumi (10).

## IN CASE THE MEDICATION DID NOT WORK

**Rudia kumeza dozi ya misoprostal tena au nenda hospitali kutumia manual vacuum aspiration** Kuna hatari ndogo sana ya kasoro za uzazi ikiwa mimba itaendelea kukua baada ya kutumia misoprostol.

## JE NILIFANIKIWA KUTOA MIMBA?

**Hata kama mwanamke anahisi hana mimba ni muhimu kuhakikisha mimba imetoka. W anawake wanatakiwa wafanye vipimo vya ujauzito au ultra sound baada ya kutoa mimba kwa kutumia misoprostol wiki 3 hadi 4 baada ya kuavya mimba**

Iwapo mwanamke hatoki damu, anatokwa na damu kidogo (chini ya hedhi na bila kuganda) na au anaendelea kuwa na dalili za ujauzito baada ya kutumia vidonge kuna uwezekano bado ni mjamzito. Anapaswa kufanya Kipimo cha picha kutumiya mawimbi ya sauti (ultrasound) haraka iwezekanavyo kuangalia kama mimba inaendelea au la, ikiwa hii haiwezekani anaweza kutumia vidonge tena.

## BAADA YA KUTOA MIMBA

Baada ya kutoa mimba mwanamke atarajie kuvuja kwa damu kidogo kwa wiki moja mpaka tatu. Lakini kila mawamke ni tofauti.baadaye mwanamke anafaa ahakikishe uavyaji wa mimba umekamilika

Wanawake wanashauriwa wasiingize kitu chochote kwenye uke, wala kufanya ngono mpaka damu iache kutoka ukeni. inakadiriwa siku 2 baada ya kutoa mimba

**Mwanamke anaweza kupata mimba mara tu baada ya kutoa mimba** Kama hataki kupata mimba kwa haraka inabidi utumie dawa za kupanga uzazi kuhakikisha hapati mimba nyingine isiyotarajiwa

## CONTACTS

Women HelpWomen
WEB: HTTPS://WOMENHELP.ORG/
EMAIL: INFO@WOMENHELP.ORG
TWITTER: @WOMENHELPORG
FACEBOOK: WOMENHELPWOMENINTERNATIONAL

MAMA Network: Mobilizing Activists around Medical Abortion (MAMA).
WEB: WWW.MAMANETWORK.ORG



## JE, MISOPROSTOL NI NINI?

Ni Dawa inayotumika dunia mzima kutoa mimba na kutibu vidonda vya tumbo. Inauzwa katika maduka ya madawa kwa majina haya: cytote,isovent,misoclear misofem,. Katika nchi nyingi za Afrika imesajiliwa kutibu na kuzuia uvujaji wa damu nyingi pindi mwanamke anapojifungua.

women help women

## MATUMIZI YA MISOPROSTAL

Utoaji mimba ulio salama, kutibu mwanamke aliyepoteza mimba Kutibu mwanamke aliyetoa mimba (kumalizia utoaji mimba usiokamilika)

Kuzuia na kutibu utvujaji mwingi wa damu baada ya kujifungua

kutibu vidonda vya tumbo(Gastric Ulcers)

## INAFANYAJE KAZI?

Misoprostol hufanya uterasi kusinyaa, kulainisha na kufungua seviksi, ambayo husababisha mchakato kama kuharibika kwa mimba.

## NI LINI INAWEZA KUTUMIKA KUTOA MIMBA SALAMA?

12 WIKI

Katika wiki was kumi na mbili (12 weeks) za kwanza za ujauzito kuhesabu kuanzia siku ya kwanza ya mzunguko wa mwisho wa hedhi.

## INATUMIKA VIPI KWENYE UTOAJI MIMBA ULIO SALAMA?

Kijumla Mwanamke anahitaji vidonge kumi na mbili vitakavyotumiwa kwa dozi ya vidonge vine (4) kila baada ya masaa matatu (3).

3 saa

Weka vidonge vinne (4) vya misoprostol chini ya ulimi

30 dakika — kwa dakika thelathini

Usivimeze, viache viyeyuke mpaka viishe

Baada ya masaa matatu weka vidonge vingine vinne (4) chini ya ulimi

30 dakika — kwa dakika thelathini

Usivimeze, viache viyeyuke mpaka viishe

Baada ya masaa matatu weka vidonge vingine vine (4) chini ya ulimi

30 dakika — kwa dakika thelathini

Usivimeze, viache viyeyuke mpaka viishe

**Ikiwa utoaji mimba haujatokea masaa matatu (3hrs) baadaye, inawezekana kutumia dozi za ziada kila baada ya masaa matatu (3) hadi kutoka kwa mimba.**

## NI NINI KINACHOTARAJIWA BAAADA YA KUTUMIA HIZO DAWA?

| | | |
|---|---|---|
| Maumivu na kutokwa damu Zaidi kuliko inavyotaki-kana wakati wa hedhi. | Kwenye asilimia 80% ya kesi za namna hii, mimba hutoka kwenye masaa 24 ya mwanzo | Kuna uwezekano kuwa maumivu yatakuwa makali zaidi na atatokwa na damu zaidi kulingana na umri wa ujauzito wake |

Dawa za kutuliza maumivu zinaweza kuchukuliwa kwa wakati mmoja na dozi ya kwanza ya Misoprostol. **Ibuprofen** ndio yenye ufanisi zaidi. **Paracetamol / acetaminophen** inaweza kutumika kwa kuongeza.



## MADHARA YANAYOTARAJIWA

30 saa

Ndani ya masaa 24 ya mwanzo mwanamke anaweza kupata dalili zifuatazo: kichefuchefu, kutapika, kuharisha kupata homa, kuumwa na kichwa au kusikia kizunguzungu. Hizi dalili hazina madhara na zitaisha ndani ya masaa machache

## ZIPI NI DALILI ZA (MADHARA) HATARISHI?

Kuvuja kwa damu nyingi (pedi mbili au tatu kujaa kwa  zaidi yaya masaa mawili au matatu zikifuatana) 2h +

39º Kupatwa na joto jingi mwilini ya celcius 38 au 39 kwa zaidi ya masaa 24 24h +

Maumivu makali yasiyotibika au kupunguzwa kwa dawa za maumivu siku chache baada ya kumeza dawa hizo

Kutokwa na uchafu unaonuka usio wa kawaida.

## NINI CHA KUFANYA YANAPOTOKEA MATATIZO?

**Nenda mara moja kwenye kituo cha afya**

**Ikitokea dharura, mhudumu wa afya ana wajibu wa kumuhudumia mhusika kwa wakati. Matibabu ya matatizo** baada ya kutumia misoprostol **ni sawa** na na matibabu ya matatizo baada ya mimba kuporomoka yenyewe. **Siyo rahisi kuona tofauti kati** ya mimba iliyo poromoka yenyewe na uavyaji  wa mimba ikitumia misoprostol. **Mwanamke anayehitaji huduma ya kiafya anaweza kusema** mimba imeporomoka yenyewe